

HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE

Simu: 028-2227148
Fax: 028-2227140



S. L. P. 20,
KARAGWE.

E-mail: ded@karagwedc.go.tz

20 JUNI 2022.

TANGAZO LA KUJENGA NA KUPANGISHWA VIBANDA VYA BIASHARA KATIKA UWANJA WA STENDI YA KAYANGA HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE.

KWA; WANANCHI WOTE.

1. Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe inawatangazia wananchi wote wenye uwezo na sifa za kufanya biashara kuleta maombi yao ya kujenga na kupangishwa vibanda vya Biashara kwa mkataba wa muda mrefu (miaka 6 na miezi 3) katika eneo la uwanja wa stendi ya Kayanga kwa mchanganuo ufuatazo:-

Na.	Jina la Zabuni	Idadi	Namba ya Zabuni
1.	Vibanda vya Maduka	136	LGA.033/2022/2023/NCS/03 LOT 1
2.	Vibanda vya Chakula	20	LGA.033/2022/2023/NCS/03 LOT 2

MASHARTI NA VIGEZO KWA WAOMBAJI;

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania (weka nakala ya kitambulisho cha mpiga kura au NIDA au Leseni ya udereva au cheti cha kuzaliwa).
 2. Kulipa ada ya maombi ya zabuni **Tsh.20,000.00 kwa kila zabuni**, ambayo haitarudishwa.
 3. Ambatanisha nakala ya listi ya malipo.
 4. Gharama za ujenzi kwa kila kibanda haitazidi **Tsh.7,500,000.00** na ujenzi utasimamiwa na Mhandisi wa ujenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe.
 5. Muda wa ujenzi ni **miezi 3** na unapaswa kukamilika kabla au ifikapo tarehe **30.09.2022**.
 6. Fika Ofisi ya ununuzi na Ugavi Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kuchukua fomu ya maombi ya ujenzi wa vibanda.
 7. Weka nakala mbili za kotesheni (Fomu) kwenye bahasha; nakala halisi na kivuli kisha funga bahasha na kuandika juu ya bahasha namba ya zabuni unayoomba na kuituma kwa; **Katibu Bodi ya Zabuni, S.L.P 20, Karagwe.** Unaruhusiwa kuomba vibanda kuanzia 1 hadi 5 tu.
 8. Halmashauri itaanza kukusanya kodi ya pango kuanzia tarehe **01.10.2022** na kodi ya pango kwa kibanda ni **Tsh.100,000.00** kwa mwezi na mpangaji atalazimika kulipa **Tsh.20,000.00** tu kila mwezi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ikiwa ni sehemu ya punguzo la pango la jumla. Aidha, makato ya kodi yatadumu kwa muda wa miezi 75 (Miaka 6 na Miezi 3) tu na mpangaji akitaka kuendelea ataruhusiwa kwa kutuma maombi mapya. Bei ya pango yaweza badilika kulingana na mabadiliko ya bei.
 9. Mpangaji atakayeshindwa kukamilisha ujenzi kwa muda wa miezi 3 iliyopangwa, atanyang'anywa umiliki wa kibanda na kupatiwa mwombaji mwingine na **Halmashauri haitahusika kurudisha gharama zake.**
 10. Mpangaji atahusika moja kwa moja kutunza mazingira katika usafi wa eneo la kibanda.
- Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 27.06.2022 Jumatatu saa 8:00 Mchana.** Maombi yote yatafunguliwa hadharani katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kuanzia saa 8:00 Mchana, waombaji wote mnakaribishwa. **Maombi yatakayochelewa hayatafunguliwa.**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KARAGWE**

Michael F Nzyungu

MKURUGENZI MTENDAJI (W) KARAGWE.

